

Madokezo ya Kujifunza Lugha


1 UWE NA KUSUDI

“Andika orodha ya sababu za kujifunza lugha mpya, halafu uipitie kila wakati unapohisi umekata tamaa.”—Serina.

Ni lugha gani ambayo ungependa kujifunza, na kwa nini?

Lugha:

Sababu:



2 UWE NA WATU WA KUKUSAIDIA


Orodhesha majina ya watu ambao utawaomba msaada utakapokabili changamoto.

“Nilipokuwa nikijifunza Kihispania, nilikuwa na watu wa kunisaidia ambao pia walikuwa wakijifunza lugha hiyo, hivyo tungeweza kutiana moyo. Niliwauliza changamoto walizokabili na jinsi walivyozitatua.”—Helena.

“Hutaweza kuzungumza lugha kwa ufasaha ikiwa huizungumzi kwa ukawaida.”—Christopher.



3 PAMBANA NA VIVUNJA MOYO



“Siku moja unahisi ni kana kwamba umeijua vizuri lugha hiyo, halafu siku nyingine unahisi hujui lolote!”—Vivian.

Ni malengo gani madogomadogo ambayo ni rahisi kuyafikia unayoweza kujiwekea yatakayokusaidia kuepuka vivunja moyo?

**“Usikate tamaa wengine wanapofanikiwa haraka kuliko wewe. Uwezo wa watu unatofautiana.”
—Thomas.**

4 FANYA MAZOEZI KILA SIKU

“Ikiwa utafanya mazoezi kwa bidii, utaelewa lugha haraka. Hata hivyo, ikiwa hufanyi mazoezi, hutafanya maendeleo haraka.”—Danielle.

Andika muda utakaotumia kila siku kujifunza lugha mpya.

Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi	Jumapili

5 IGA UTAMADUNI

*“Mimi hujaribu kujifunza kuhusu watu wanaozungumza lugha ninayojifunza. Ninatambua jinsi wanavyofanya mambo, ninajaribu kula vyakula wanavyopenda, na ninasikiliza miziki yao. Kujifunza lugha kunahusisha mengi zaidi ya kuizungumza!”
—Alexis.*

Utafanya nini ili uige utamaduni wa watu ambao unajifunza lugha yao?

6 TEMBELEA NCHI YAO

*“Tulitembelea Chile kwa miezi minane, na tulijifunza Kihispania haraka kwa sababu tulisikia watu wakizungumza lugha hiyo kila siku.”
—Natasha.*

Onyesha nchi ambayo ungependa kutembelea.



*“Tumia wakati kusoma, kuandika, kuzungumza, na kusikiliza. Ili uzungumze lugha kwa ufasaha unahitaji kufanya mambo hayo manne.”
—Allison.*

Iwe utaenda nchi nyingine
au la, unaweza kwenda wapi
ili uchagamane na watu
wanaozungumza lugha
unayojifunza?